BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Pili – Tarehe 08 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

18. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakialikwa kuhudhuria shughuli mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo kumekuwa na mazoea ya kutowatambua pale wanapohudhuria kwenye hafla hizo kwa kuwataja tu kama nao wamehudhuria.

(a) Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ni Mhimili kati ya

Mihimili mitatu ya nchi yetu na Wajumbe wake wanawawakilisha wananchi wa Zanzibar, je ni lini Serikali itachukuwa hatua ya kuwatambulisha Wajumbe hao kama ilivyo kwa nchi nyengine.

(b) Hivi ni gharama kiasi gani Serikali itaingia iwapo itawatambua kuwepo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika shughuli zake.

<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

85. MHESHIMIWA ZAINA ABDULLA SALUM (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi kubwa za kuinua viwango vya mishahara kwa wafanyakazi wote wa umma. Hata hivyo, kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto kubwa katika Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali, kuchelewa au kushindwa kabisa kuwasilisha katika Wizara yako, taarifa za wafanyakazi walio katika Wizara au Taasisi hizo ambao wameshafariki, waliochukua likizo bila ya malipo au kufukuzwa kazi, hali inayopelekea Serikali kuendelea kulipa mishahara hewa wakati wafanyakazi hao hawatumikii tena utumishi wa Wizara na Taasisi hizo.

(a) Je, ni sababu gani zinazozipelekea baadhi ya Wizara naTaasisi za Serikali kushindwa au kuchelewa kuwasilisha taarifa za watumishi wao waliofariki, kuchukua likizo bila ya malipo au kufukuzwa kazi kwenye Wizara yako kwa wakati.

(b) Je, Wizara yako inachukua hatua gani kwa Wizara na Taasisi zinazokucheleweshea au kushindwa kabisa kukuwasilishia taarifa za wafanyakazi wao waliofariki, kuchukua likizo bila ya malipo au kufukuzwa kazi kwa wakati.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

30. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Wastaafu ni watu ambao wameshatoa michango yao mingi na mikubwa kwa maslahi ya Taifa. Hata hivyo, watu hawa wanaendelea kuishi katika mazingira magumu

yanayosababishwa na mfumuko wa bei na ughali wa maisha.

Je, ni lini Serikali kupitia Wizara yako imedhamiria kuboresha maslahi ya wastaafu kupitia huduma ya Pencheni.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

58. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa zaidi ya asilimia 80, ya Wanzanzibari wanategemea usafiri pamoja na usafirishaji wa baharini. Na kwakuwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi leo hii haijaanzisha chuo maalum kinachofundisha vijana wetu taaluma ya Uhandisi na Uongozi wa Vyombo vya Baharini (Marine Navigation and Engineering).

Je, ni lini Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaanzisha kitengo cha Uhandisi pamoja na Uongozaji wa vyombo vya baharini katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

63. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika jimbo la Mtambile kuna bonde maarufu la Mtambile Machigini ambalo wananchi wa jimbo hilo hulitumia kwa shughuli za kilimo ambalo kimsingi lina hadhi sawa na mabonde ya kilimo cha mpunga ya Mlemele.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima katika uendelezwaji wa bonde hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

12. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika Shehia ya Kengeja lipo jengo la Posta na kwa muda mrefu sasa jengo hilo halitumiki.

(a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya matumizi ya jengo hilo.

(b) Ni sababu gani zilizopelekea jengo hilo kutokutumika hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa teknolojia imezidi kuendelea.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

66. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ndani ya jimbo la Wingwi kuna madiko matatu (yaani Kicheche, Tanda Tumbi na Sizini) ambayo yanatumiwa na wavuvi wa maeneo ya Wingwi na Sizini kuuzia samaki wao. Hata hivyo kuna wasiwasi kwamba madiko haya hayajapewa hadhi yake.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inayatambua madiko hayo.

(b) Je, ni lini Serikali itaanza rasmi kupeleka watendaji wake kwa lengo la kukusanya mapato kupitia madiko hayo pamoja na kuongeza ajira kwa wananchi wakiwemo watu wa jimbo la Wingwi.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuyaendeleza madiko haya na mfano wa haya.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

27. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini

Wananchi wa vijiji vya Mwakaje na Mwache Alale, wamekuwa wakipata shida kubwa ya maji pamoja na juhudi za Serikali kuchimba kisima katika kijiji cha Mwache Alale kupitia mradi wa Ras el Hema. Kisima hicho kiliwapa matumaini wananchi wa maeneo hayo kwamba shida hiyo ya maji inayowakabili kwa muda mrefu itaisha hivi karibuni, lakini hadi muda huu zaidi ya miaka mitano imepita kisima hicho bado hakijakamilika.
Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa vijiji hivyo katika kukimalizia kisima hicho na kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi hao.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

40. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ya kuikuza sekta ya Utalii hapa nchini, baadhi ya maeneo yanayotumika kwa shughuli za utalii hasa sehemu za ufukweni, yanalindwa na Askari wanaotembea na silaha za moto (Bunduki), kitu ambacho kinaweza kupunguza shughuli za kitalii nchini, ikizingatiwa kuwa ipo sheria inayowaongoza vizuri na haina athari hasa kwa kuendesha vizuri kazi za ulinzi kwa vikosi vyetu.

Je, Serikali kupitia Wizara hii imejipangaje kuondosha changamoto hiyo.

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

35. Mheshimiwa Saada Ramadhan Mwendwa (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ofisi za Wakuu wa Wilaya zimekuwa na vitengo vya uratibu wa malezi ya walezi hali ambayo imesababisha kuteuliwa kwa waratibu wa malezi ya walezi kwa kila shehia. Hata hivyo, waratibu hawa wa shehia wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kukosa vitendea kazi na kutokulipwa posho kwa kazi yao hiyo, hali inayowapelekea kuishi maisha magumu kutokana na uchache wa kipato chao.

(a) Kwa kuwa Serikali inawatambua waratibu hao na kwa kuwa waratibu wanafanyakazi hasa kuwahifadhi watoto waliopotea katika mazingira hatarishi, je ni lini Serikali itatoa angalau posho kwa waratibu hao.

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika katika kuwateuwa waratibu hawa.

III. <u>HOJA ZA SERIKALI</u>

<u>**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.**</u>

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Zanzibar,
08 Septemba, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.